**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# FOMATI YA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (STANDARD FOUR NATIONAL ASSESSMENT FORMAT – SFNA)

**IMETOLEWA NA:**

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
S.L.P. 2624
DAR ES SALAAM
TANZANIA

MEI, 2015

Limechapishwa na
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2015

Haki zote zimehifadhiwa.

# Yaliyomo


DIBAJI ....................................................................................iv

01 KISWAHILI .............................................................................1

02 ENGLISH LANGUAGE ...........................................................4

03 MAARIFA YA JAMII…………………………………………...8

04 HISABATI ...........................................................................13

05 SAYANSI .............................................................................15

06 STADI ZA KAZI, HAIBA NA MICHEZO ...............................18

07 TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA) ....................................................................22

# DIBAJI

Fomati hii ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne imeandaliwa kwa kuzingatia Mihitasari ya **mwaka 2005** iliyoanza kutumika Januari **2007**. Aidha, fomati hii imezingatia mabadiliko ya msingi ya upimaji wenye mtazamo wa mhamo wa ruwaza kwa kupima ujuzi, stadi na mielekeo mbalimbali aliyojifunza mtahiniwa. Upimaji utazingatia pia jinsi mtahiniwa anavyoweza kumudu stadi za Kusoma, Kuandika, Kuhesabu na kutumia ujuzi aliopata katika kutatua matatizo ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiteknolojia.

Katika mtaala mpya masomo yanayofundishwa ni **kumi na moja** kama ilivyobainishwa katika Waraka wa Elimu Na. 2 wa Mwaka 2006 wenye **Kumb. Na. ED/CK/C.2/4/V/2** wa tarehe **04/04/2006**. Masomo hayo ni **Kiswahili, English Language, Uraia, Historia, Jiografia, Stadi za Kazi, Hisabati, Sayansi, Haiba na Michezo**, **Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)**, **Haiba na Michezo** na **Kifaransa**. Kati ya masomo haya, masomo ya lazima ni **Kiswahili**, **English Language**, **Uraia**, **Historia**, **Jiografia**, **Stadi za Kazi**, **Hisabati**, **Sayansi** na **Haiba na Michezo**. Masomo ya **Kifaransa** na **Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)** yatakuwa masomo ya hiari.

Katika Fomati hii baadhi ya masomo yatatahiniwa kwa kuunganishwa kutokana na uhusiano uliopo. Masomo hayo ni Uraia, Historia na Jiografia ambayo yatatahiniwa kama Maarifa ya Jamii. Aidha masomo ya Stadi za Kazi na Haiba na Michezo pia yataunganishwa na kuwa na karatasi moja ya mtihani. Hivyo masomo yatakayotaniwa katika Darasa la Nne ni Maarifa ya Jamii, Kiswahili, English Language, Hisabati, Sayansi, Stadi za Kazi, Haiba na Michezo na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Aidha somo la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) litakuwa kwa wanafunzi wenye walimu na vifaa watakaosajili kufanya somo hilo.

Fomati hii imeandaliwa kwa kuzingatia mada zilizomo katika mihtasari mipya inayofundishwa katika Shule za Msingi Darasa la Nne na itaanza kutumika kupima watahiniwa kuanzia mwaka 2015. Fomati hii inatoa mwongozo kwa walimu na wanafunzi kuhusu muundo wa karatasi ya upimaji kwa kila somo. Walimu na wanafunzi wanashauriwa kutotumia fomati hii kama mbadala wa mihutasari. Katika ufundishaji na ujifunzaji ni lazima mada zote zilizoainishwa katika mihutasari ya shule za msingi katika Darasa la Nne zifundishwe kikamilifu.

Fomati ya kila somo inaonesha Utangulizi, Malengo ya Jumla, Ujuzi wa Jumla, Muundo wa karatasi ya upimaji na Mada zitakazotahiniwa. Muda wa upimaji kwa kila somo umeoneshwa. Watahiniwa wasioona wataongezewa muda wa ziada wa dakika 10 kwa kila saa kwa masomo ya Lugha, Sanaa na Sayansi, na katika somo la Hisabati watahiniwa wataongezewa dakika 20 kwa kila saa.

Baraza la Mitihani linatoa shukrani za dhati kwa Maafisa Mitihani na wote walioshiriki katika kuandaa fomati hii. Aidha Baraza la Mitihani litakuwa tayari kupokea ushauri, maoni na mapendekezo kutoka kwa wadau wa elimu kuhusu fomati hizi kwa lengo la kuziboresha.

Dkt. Charles E. Msonde
**Katibu Mtendaji**

# 01 KISWAHILI

## 1.0 UTANGULIZI

Fomati hii ya upimaji wa somo la Kiswahili inatokana na Muhtasari wa somo la Kiswahili wa mwaka 2005 ulioanza kutumika Januari 2007. Muhtasari huo uliboreshwa kwa kuzingatia mabadiliko ya msingi yaliyofanywa katika Mtaala.

Fomati hii ya upimaji wa somo la Kiswahili itapima ujuzi, stadi na mielekeo mbalimbali aliyojifunza mtahiniwa badala ya kuweka mkazo katika upimaji wa namna mtahiniwa alivyomudu maudhui za mada mbalimbali zilizoainishwa kwenye muhtasari.

## 2.0 MALENGO YA JUMLA

Upimaji wa somo la Kiswahili unalenga katika kupima uwezo wa mtahiniwa katika:

2.1 Kutumia Kiswahili fasaha katika hali na miktadha mbalimbali kwa kuzungumza, kusoma na kuandika.
2.2 Kuwasiliana kwa kutumia sarufi ya Kiswahili Sanifu.
2.3 Kupata misingi bora na imara ya kujifunza kwa ajili ya kujiendeleza.
2.4 Kutumia lugha ya kisanii katika miktadha mbalimbali.
2.5 Kuthamini Kiswahili kama ni sehemu ya utamaduni wa Mtanzania.

## 3.0 UJUZI WA JUMLA

Upimaji wa jumla unalenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika:

3.1 Kuzungumza na kuandika Kiswahili kwa ufasaha ili kukidhi mahitaji ya msingi ya mtumiaji wa lugha ya Kiswahili.
3.2 Kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili katika shughuli za kila siku katika miktadha na mazingira mbalimbali.
3.3 Kusikiliza, kusoma na kuandika sentensi na habari fupi.
3.4 Kukipenda na kukithamini Kiswahili kama lugha ya Taifa na ya Kimataifa.
3.5 Kutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano.
3.6 Kusoma kwa ufahamu na kwa burudani.

3.7 Kujisomea maandiko ya kiada na ziada kwa ufahamu, kupata maarifa na kwa burudani.

## 4.0 MUUNDO WA KARATASI YA UPIMAJI

4.1 Upimaji wa Kiswahili utakuwa na sehemu A, B, C na D. Sehemu A itahusisha mada ya Kusoma kwa Utambuzi na Kuandika, sehemu B itahusisha mada ya Sarufi na Utumizi wa Lugha, sehemu C itahusisha mada ya Lugha ya Kifasihi na sehemu D itahusisha mada ya Ufahamu.

4.2 Karatasi ya upimaji itakuwa na jumla ya maswali **ishirini na tano (25)**.

4.3 Muda wa upimaji utakuwa saa **1:00** ambapo watahiniwa wasioona watapimwa kwa muda wa saa **1:10**.

### 4.4 SEHEMU A: IMLA

Sehemu hii itakuwa na maswali **matano (05)**. Mtahiniwa atatakiwa kusikiliza sentensi zitakazosomwa na kisha kuziandika. Kila swali litakuwa na alama **mbili (02)** na hivyo kufanya jumla ya alama **kumi (10)** katika sehemu hii.

### 4.5 SEHEMU B: SARUFI

4.5.1 Sehemu hii itakuwa na maswali **matano (05)** ya kuchagua jibu sahihi kutoka katika chaguzi A, B, C na D. Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **yote**. Kila swali litakuwa na alama **mbili (02)** na kufanya jumla ya alama **kumi (10)** katika sehemu hii.

4.5.2 Maswali yatajikita katika kutaja majina ya vitu katika umoja na wingi, utambulisho, kueleza matukio kwa kutumia nyakati mbalimbali, kueleza undugu, kueleza matukio katika hali mbalimbali, kulinganisha na kutofautisha vitu na kubainisha maana za misamiati.

### 4.6 SEHEMU C: LUGHA YA KIFASIHI

4.6.1 Sehemu hii itakuwa na maswali **kumi (10)** ya kujaza nafasi zilizo wazi. Mtahiniwa atatakiwa kujibu

maswali **yote**. Kila swali litakuwa na alama **mbili (02)** na kufanya jumla ya alama **ishirini (20)** katika sehemu hii.

4.6.2 Maswali **matano (05)** yatakuwa ya kukamilisha nafasi zilizo wazi kwa kuandika majibu sahihi na maswali mengine **matano (05)** yatakuwa ya kukamilisha nafasi zilizo wazi kwa kutumia maneno yaliyopo kwenye kisanduku.

4.6.3 Maswali yatajikita katika mada ndogo za methali, nahau na vitendawili.

### 4.7 SEHEMU D: UFAHAMU

4.7.1 Sehemu hii itakuwa na maswali **matano (05)** na mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **yote**. Kila swali litakuwa na alama **mbili (02)** na kufanya jumla ya alama **kumi (10)** katika sehemu hii.

4.7.2 Maswali yatakuwa ya kuchagua jibu sahihi katika chaguzi A, B, C na D au kuandika jibu sahihi kutokana na habari aliyoisoma.

4.7.3 Maswali yatajikita katika ufahamu wa kusoma habari au mashairi.

## 5.0 MADA ZITAKAZOPIMWA

Mada zifuatazo zitapimwa:

5.1 Kusoma kwa Utambuzi na Kuandika

5.2 Sarufi na Utumizi wa Lugha

5.3 Lugha ya Kifasihi

5.4 Ufahamu.

# 02 ENGLISH LANGUAGE

## 1.0 INTRODUCTION

This assessment format for Standard Four is based on the English Language syllabus of 2005 which was used for the first time in 2007. The English Language syllabus was prepared by considering the changes of paradigm shift from content to competence based type of teaching and learning as effected in the curriculum.

This format aims at assessing candidates' competences, skills and attitudes in learning. The examination will assess how candidates use the attained competences and take part in simple conversations.

## 2.0 GENERAL OBJECTIVES

The English assessment aims at testing candidates' ability to:

2.1 Listen to a dictation and write the given words/sentences correctly.

2.2 Write simple grammatically correct sentences.

2.3 Read and complete sentences using correct English.

2.4 Read and comprehend a simple passage.

## 3.0 GENERAL COMPETENCES

The English assessment will measure the candidates' competences on how to:

3.1 Express themselves appropriately in family, school and local environment settings and situations.

3.2 Communicate in simple routine tasks requiring simple exchange of information using all the four language skills.

## 4.0 COMPOSITION OF ASSESSMENT PAPER

4.1 The English assessment paper will consist of sections A, B, C and D. Section A will be on Dictation, Section B on Vocabulary, Section C on Grammar and Section D on Comprehension.

4.2 The assessment paper will have a total of **twenty five (25)** questions which will carry **two (02)** marks each, making a total of **fifty (50)** marks.

4.3 Candidates will be required to answer **all** questions.

4.4 This paper will take **1:00 hour**. The candidates with Visual Impairment will take **1:10 hours**.

### 4.5 SECTION A: DICTATION

4.5.1 This section will comprise of **five simple sentences** for questions 1, 2, 3, 4 and 5 to be dictated to pupils by a teacher. Each question will carry **two (02)** marks making a total of **ten (10)** marks in this section.

4.5.2 Candidates are required to listen and write the simple sentences dictated in the spaces provided correctly.

### 4.6 SECTION B: VOCABULARY

4.6.1 This section will comprise **five (05)** multiple choice questions. Each question will carry **two (02)** marks making a total of **ten (10)** marks in this section.

4.6.2 Candidates will be required to answer **all** questions by choosing the correct answer from options A, B, C and D.

4.7 **SECTION C: GRAMMAR**

4.7.1 This section will comprise of **two parts, A and B. Part A** will be on other forms of Grammar and will have **five (05)** filling-in the blank spaces questions with a choice of words provided in the box. **Part B** will be on Tenses and will also have **five (05)** filling-in the blank spaces questions using the correct form of the words in brackets. There will be a total of **10** questions in both parts A and B. Each question will carry **two (02)** marks making a total of **twenty (20)** marks in this section.

4.7.2 Candidates will be required to answer **all** questions by filling in the blank spaces with correct words.

4.8 **SECTION D: COMPREHENSION**

4.8.1 This section will comprise of a short passage which will be followed by **five (05)** questions which will either be multiple choice, gap filling or Wh-questions. Each question will carry **two (02)** marks making a total of **ten (10)** marks in this section.

4.8.2 Candidates will be required to answer **all** questions using the information from the passage.

## 5.0 TOPICS TO BE ASSESSED

The following topics will be assessed:

5.1 Dictation
5.2 Vocabulary
5.3 Tenses
5.4 Other forms of Grammar
5.5 Comprehension.

## 03 MAARIFA YA JAMII

## 1.0 UTANGULIZI

Fomati hii ya somo la Maarifa ya Jamii inatokana na mihutasari ya masomo ya Historia, Uraia na Jiografia ya mwaka 2006 iliyoanza kutumika Januari 2007. Fomati hii inazingatia malengo ya mitaala ya elimu ya msingi ambayo ni kupima ujuzi, stadi na mielekeo mbali mbali aliyojifunza mtahiniwa wa elimu ya msingi kwa ngazi ya Darasa la Nne.

Upimaji wa somo la Maarifa ya Jamii utakuwa na karatasi moja yenye masomo ya Historia, Uraia na Jiografia.

Katika kuandaa fomati hii, kila somo limepewa uzito kulingana na mada watahiniwa wanazotakiwa kujifunza kwa kipindi husika kwa masomo yote matatu.

## 2.0 MALENGO YA JUMLA

Upimaji wa somo la Maarifa ya Jamii (Historia, Uraia na Jiografia) unalenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika:

2.1 Kufahamu chimbuko la familia zao, ukoo, kijiji, mtaa na shule zao.

2.2 Kuelewa mahusiano ya kijamii na kiuchumi katika familia, ukoo, kijiji, mtaa na shule.

2.3 Kuelewa hatua za maendeleo katika familia, ukoo, kijiji, mtaa na shule tangu kuwepo kwake.

2.4 Kukusanya taarifa za kihistoria za familia, ukoo, kijiji, mtaa na shule na kuziwasilisha darasani.

2.5 Kubaini na kuthamini maeneo ya kihistoria katika kijiji au mtaa.

2.6 Kuelewa chimbuko la binadamu na mabadiliko yake ya kimaumbile katika zama mbalimbali.

2.7 Kuelewa kiyakinifu hatua mbalimbali za maendeleo ya kiuchumi na kijamii alizopitia binadamu katika zama mbalimbali.

2.8 Kuchanganua mahusiano ya kijamii na kiuchumi miongoni mwa watanzania katika nyakati mbalimbali.

2.9 Kufahamu na kuthamini misingi na dhima ya mila na desturi za jamii yake katika nyakati mbalimbali.

2.10 Kuelewa na kuheshimu dhana ya uongozi katika familia na shule.

2.11 Kutambua, kuthamini na kuheshimu alama za utambulisho wa shule na taifa letu.

2.12 Kuelewa misingi ya demokrasia, haki za watoto, utawala bora, muundo na taratibu za uundaji na uendeshaji wa serikali ya mitaa/kijiji.

2.13 Kutambua na kuimarisha juhudi za kudumisha ulinzi na usalama katika familia na shule.

2.14 Kubaini na kutafsiri mazingira yanayomzunguka.

2.15 Kutambua na kutumia stadi sahili za picha na ramani katika kutafsiri na kuyaelewa mazingira.

2.16 Kubaini njia anuai za kutunza, kuhifadhi na kutumia mazingira yanayomzunguka kwa njia endelevu kwa kushirikiana na wanajamii wengine.

2.17 Kutambua mabadiliko ya hali ya hewa na kubaini umuhimu wake.

## 3.0 UJUZI WA JUMLA

Upimaji unalenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika:

3.1 Kuthamini chimbuko la familia, ukoo, kijiji, mtaa na shule zao ili wajione kama ni sehemu ya jamii hizo.

3.2 Kushiriki katika shughuli mbalimbali kama sehemu ya familia, ukoo, kijiji, mtaa na shule ili kutekeleza kikamilifu wajibu wao kwa jamii.

3.3 Kuelewa kiyakinifu maendeleo yaliyofikiwa katika familia, ukoo, kijiji, mtaa na shule katika nyakati mbalimbali kwa nia ya kuyaenzi na kuyaendeleza.

3.4 Kutambua chimbuko na mabadiliko ya binadamu ya kimaumbile, kijamii na kiuchumi tangu kuwepo kwake ili kuyatathmini na kuyaeleza kimantiki.

3.5 Kung’amua na kuthamini mila na desturi za jamii yake ili aendeleze zile zinazofaa.

3.6 Kutafuta, kukusanya na kuchambua taarifa za kihistoria ili kuzitumia katika kujenga, kutetea hoja na kujiendeleza kitaaluma.

3.7 Kutafuta, kuchambua na kutafsiri taarifa zinazohusu masuala ya uongozi wa kijamii katika ngazi ya familia shule na kijiji au mtaa.

3.8 Kuheshimu mamlaka na kushiriki katika kukuza demokrasia na haki za binadamu katika ngazi ya shule na kijiji/mtaa.

3.9 Kutafsiri, kuthamini na kuheshimu alama za shule na Taifa letu.

3.10 Masuala yanayohusiana na ulinzi na usalama katika ngazi ya familia na shule.

3.11 Kuchora, kutengeneza, kuunda na kujenga ramani kwa kutumia vipengele muhimu vya ramani.

3.12 Kutambua mipaka, sura ya nchi, uoto na viumbe hai katika tarafa, wilaya yake na nchi yake.

3.13 Kuelewa matumizi mbalimbali ya mazingira na jinsi ya kuyajifadhi na kuyatunza katika tarafa, wilaya yake na nchi yake.

3.14 Kuelewa maana ya hali ya hewa, vipengele vinavyounda hali ya hewa, kupima na kurekodi vipengele hivyo na kutafisri matokeo hayo na kuyatumia.

## 4.0 MUUNDO WA KARATASI YA UPIMAJI

4.1 Upimaji wa somo la Maarifa ya Jamii utakuwa na sehemu A, B na C. Sehemu A itahusisha mtihani wa somo la Historia, Sehemu B Uraia na Sehemu C Jiografia.

4.2 Upimaji utakuwa na jumla ya maswali **ishirini na tano (25)**.

4.3 Muda wa kufanya upimaji utakuwa saa **1:00**. Aidha, watahiniwa wasioona watapimwa kwa muda wa saa **1:10**.

### 4.4 SEHEMU A: HISTORIA

4.4.1 Sehemu ya Historia itakuwa na maswali **saba (07)**.

4.6.2 Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **yote**. Kila swali litakuwa na alama **mbili (02)** na hivyo kufanya jumla ya alama **kumi na nne (14)** katika sehemu hii.

4.6.3 Maswali katika sehemu hii yatakuwa ya kuchagua jibu sahihi na kukamilisha sentensi kwa kuandika jibu sahihi au kujaza KWELI au SI KWELI.

### 4.7 SEHEMU B: URAIA

4.7.1 Sehemu ya Uraia itakuwa na maswali **saba (07)**. Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **yote**. Kila swali litakuwa na alama **mbili (02)** na kufanya jumla ya alama **kumi na nne (14)** katika sehemu hii.

4.7.2 Maswali katika sehemu hii, yatakuwa ya kuchagua jibu sahihi, kukamilisha sentensi kwa

kuandika jibu sahihi na kujaza KWELI au SI KWELI.

4.8 **SEHEMU C: JIOGRAFIA**

4.7.3 Sehemu ya Jiografia itakuwa na jumla ya maswali **kumi na moja (11)**. Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **yote**. Kila swali litakuwa na alama **mbili (02)** na kufanya jumla ya alama **ishirini na mbili (22**) katika sehemu hii.

4.7.4 Maswali yatakuwa ya kuchagua jibu sahihi, kukamilisha sentensi kwa kuandika jibu sahihi na kuoanisha sentensi na jibu sahihi.

## 5.0 MADA ZITAKAZOPIMWA

Mada zitakazopimwa katika somo la Maarifa ya Jamii ni kama ifuatavyo:

5.1 **HISTORIA**

5.1.1 Familia yetu

5.1.2 Ukoo wetu

5.1.3 Shule yetu

5.1.4 Kijiji/Mtaa wetu

5.1.5 Chimbuko na mabadiliko ya binadamu

5.1.6 Hatua za maendeleo katika zama mbalimbali

5.1.7 Kukua kwa Mifumo ya Kiuchumi na Kiutawala katika Jamii za Tanzania hadi karne ya Kumi na Tisa

5.1.8 Mahusiano Miongoni mwa Jamii za Tanzania hadi karne ya Kumi na Tisa

5.1.9 Utamaduni.

5.2 **URAIA**

5.2.1 Uongozi katika ngazi ya Familia, Shule na Serikali za Mitaa

5.2.2 Alama za Shule na za Taifa

5.2.3 Misingi ya Demokrasia

5.2.4 Ulinzi na Usalama katika ngazi ya Familia na Shule.

5.3 **JIOGRAFIA**

5.3.1 Mazingira

5.3.2 Picha

5.3.3 Ramani Rahisi

5.3.4 Uchoraji, Utengenezaji, Uundaji na Ujenzi wa Ramani

5.3.5 Hali ya hewa ya Tarafa, Wilaya na Nchi

5.3.6 Shughuli za Kiuchumi katika Tarafa, Wilaya na Nchi

5.3.7 Stadi sahili za Ramani.

# 04 HISABATI

## 1.0 UTANGULIZI

Fomati hii ya upimaji wa Darasa la Nne somo la Hisabati inatokana na muhtasari wa somo la Hisabati wa mwaka 2005 ulioanza kutumika Januari, 2007. Muhtasari huo ulioboreshwa ulitungwa kwa kuzingatia mabadiliko ya msingi yaliyofanywa katika mtaala.

Fomati hii ya mtihani imeweka Nyanja za kupima ujuzi, stadi na mielekeo mbalimbali aliyojifunza mtahiniwa badala ya kuweka mkazo katika kupima maudhui ya mada mbalimbali zilizoainishwa katika muhtasari. Aidha upimaji utazingatia jinsi mtahiniwa anavyoweza kutumia maarifa aliyopata katika kubaini mantiki za Kihisabati katika ngazi hiyo ya elimu na kutumia ujuzi huo katika kupata majibu ya maswali mbalimbali ya kihisabati yanayowiana na maisha ya kila siku.

## 2.0 MALENGO YA JUMLA

Upimaji wa somo la Hisabati kwa Darasa la Nne unalenga kubaini uwezo wa mtahiniwa katika:

2.1 Kubaini mantiki za Kihisabati katika ngazi ya elimu ya Darasa Nne.

2.2 Kutumia ujuzi aliopata katika kupata majibu ya maswali mbalimbali ya Kihisabati yanayowiana na maisha ya kila siku.

## 3.0 UJUZI WA JUMLA

Upimaji wa somo la Hisabati unalenga kubaini ujuzi wa mtahiniwa katika:

3.1 Kutambua na kufanya matendo ya Hisabati.

3.2 Kupima, kuunda na kutengeneza vifaa.

3.3 Kufumbua mafumbo kwa kufafanua, kuwianisha na kurahisisha.

3.4 Kuchora, kutafsiri data, takwimu na grafu.

## 4.0 MUUNDO WA KARATASI YA UPIMAJI

4.1 Karatasi ya upimaji itakuwa na jumla ya maswali **ishirini na tano (25)** na mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **yote**. Kila swali litakuwa na alama **mbili (02)**.

4.2 Muda wa upimaji utakuwa saa **1:30**.

4.3 Watahiniwa wasioona watapimwa kwa muda wa saa **2:00**.

## 5.0 MADA ZITAKAZOPIMWA

Mada zifuatazo zitapimwa:

5.1 Namba nzima

5.2 Sehemu

5.3 Fedha

5.4 Jometri

5.5 Vipimo

5.6 Namba za Kirumi

5.7 Takwimu.

## 05 SAYANSI

## 1.0 UTANGULIZI

Fomati hii ya upimaji wa somo la Sayansi inatokana na Muhtasari wa somo la Sayansi wa mwaka 2005 ulioanza kutumika Januari 2007 ambao ulizingatia muhamo wa ruwaza. Aidha fomati hii imezingatia malengo ya upimaji wa Elimu ya Msingi Darasa la Nne ambayo ni pamoja na kufuatilia kiwango cha ujifunzaji wa wanafunzi wa Darasa la Nne katika somo la Sayansi.

Fomati hii imeingiza mabadiliko ya msingi ya kupima ujuzi, stadi na mielekeo mbalimbali aliyojifunza mtahiniwa badala ya kuweka mkazo katika kupima namna mtahiniwa alivyomudu maudhui ya mada zilizoainishwa katika muhtasari. Aidha, upimaji utahusu jinsi mtahiniwa anavyoweza kutumia ujuzi aliopata katika kutatua changamoto mbalimbali katika mazingira anamoishi ili kupambana na changamoto zinazotokana na ujinga, maradhi na umaskini.

## 2.0 MALENGO YA JUMLA

Upimaji unalenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika:

2.1 Kudumisha usafi wa mwili, mavazi, mazingira na ubora wa chakula.
2.2 Kujikinga na magonjwa yanayoambukiza kwa njia ya hewa, maji, mavazi na kugusana na wadudu.
2.3 Kuchukua tahadhari na usalama wa matukio mbalimbali katika mazingira.
2.4 Kutoa huduma ya kwanza kwa mtu aliyezirai, aliyepatwa na matatizo ya misuli na anayetokwa na damu puani.
2.5 Kubaini mahitaji ya viumbe hai.
2.6 Kutumia maarifa ya kisayansi katika maisha ya kila siku.

## 3.0 UJUZI WA JUMLA

Upimaji utalenga kubaini ujuzi wa mtahiniwa katika:

3.1 Kumudu stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu.

3.2 Kutumia ugunduzi wa kisayansi katika kuboresha maisha ya kila siku.
3.3 Kubuni na kutumia maarifa ya kisayansi katika kutatua matatizo kwenye mazingira anamoishi.
3.4 Kutambua misingi ya Sayansi na kutumia Teknolojia kutatua matatizo ya msingi katika jamii.
3.5 Kupenda na kutumia misingi ya Sayansi na Teknolojia katika maisha ya kila siku.

## 4.0 MUUNDO WA KARATASI YA UPIMAJI

Karatasi ya upimaji itakuwa na sehemu A, B, C na D zenye jumla ya maswali **ishirini na tano (25)** na mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **yote**.

### 4.1 SEHEMU A

Sehemu hii itakuwa na maswali **kumi (10)** ya kuchagua jibu moja sahihi kati ya chaguzi A, B, C na D. Kila swali litakuwa na alama **mbili (02)** na hivyo kufanya jumla ya alama **ishirini (20)** katika sehemu hii.

### 4.2 SEHEMU B

Sehemu hii itakuwa na maswali **matano (05)** ya kuoanisha kwa usahihi dhana mbalimbali za kisayansi kulingana na matakwa ya swali. Kila swali litakuwa na alama **mbili (02)** na kufanya jumla ya alama **kumi (10)** katika sehemu hii.

### 4.3 SEHEMU C

Sehemu hii itakuwa na maswali **saba (07)** ya kujaza nafasi zilizoachwa wazi. Kila swali litakuwa na alama **mbili (02)** na kufanya jumla ya alama **kumi na nne (14)** katika sehemu hii.

### 4.4 SEHEMU D

Sehemu hii itakuwa na maswali **matatu (03)** ambayo mtahiniwa atatakiwa kuandika KWELI au SI KWELI kulingana na matakwa ya swali. Kila swali litakuwa na

alama **mbili (02)** na kufanya jumla ya alama **sita (06)** katika sehemu hii.

4.5 Upimaji utafanyika kwa muda wa saa **1:00** ambapo watahiniwa wasioona watapimwa kwa muda wa saa **1:10**.

## 5.0 MADA ZITAKAZOPIMWA

Mada zifuatazo zitapimwa:

5.1 Afya na Njia za Kujikinga na Magonjwa
5.2 VVU na UKIMWI
5.3 Huduma ya Kwanza.
5.4 Mbinu na Taratibu za Kisayansi
5.5 Viumbe Hai
5.6 Mabadiliko ya Violwa, Hali na Matukio
5.7 Nishati, Mashine na Kazi
5.8 Mahitaji Muhimu kwa Afya na Uhai.

## 06 STADI ZA KAZI, HAIBA NA MICHEZO

## 1.0 UTANGULIZI

Fomati hii ya upimaji wa somo la Stadi za Kazi, Haiba na Michezo inatokana na Mihtasari ya masomo ya Stadi za Kazi na Haiba na Michezo ya mwaka 2005 iliyoanza kutumika Januari 2007. Mihtasari hiyo iliboreshwa kwa kuzingatia mabadiliko ya msingi yaliyofanywa katika Mitaala. Aidha fomati hii ya mtihani wa Stadi za Kazi, Haiba na Michezo imeingiza mabadiliko ya msingi ya utoaji mtihani wenye kupima ujuzi, stadi na mielekeo mbalimbali aliyojifunza mtahiniwa badala ya kuweka mkazo katika upimaji wa namna mtahiniwa alivyomudu maudhui za mada mbalimbali zilizoainishwa kwenye Mihtasari.

## 2.0 MALENGO YA JUMLA

Upimaji wa somo la Stadi za Kazi, Haiba na Michezo unalenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika:

2.1 Kucheza kwa kujiburudisha, ushirikiano, kujenga mwili, upendo, kujiamini na kwa ustadi.

2.2 Kutambua amali na maadili katika jamii na kuthamini utu wake na wa wenzake.

2.3 Kufikiri kiyakinifu na ubunifu na kujiwekea mipango ya kujitegemea.

2.4 Kuelewa na kuweza kufuata misingi, kanuni na mbinu mbalimbali katika sanaa, muziki, ususi, kilimo na ufugaji, kushona na kutarizi, kupika, kufua na kupiga pasi nguo za aina mbalimbali.

2.5 Kujenga misingi ya stadi za kazi mbalimbali zitakazomwezesha mwanafunzi kujiendeleza katika maisha yake.

## 3.0 UJUZI WA JUMLA

Upimaji unalenga kubaini ujuzi wa mtahiniwa katika:

3.1 Kushiriki michezo kwa kujiburudisha, kujenga mwili, upendo, ustadi, kujiamini na kwa ushindani.

3.2 Kuzingatia amali na maadili ya jamii na kushirikiana na watu wengine katika jamii.

3.3 Kutumia stadi mbalimbali katika kukabili na kutatua matatizo.

3.4 Kuepuka vishawishi na vitendo vinavyoweza kuhatarisha maisha.

3.5 Kujenga uwezo wa kujitegemea, kujiwekea malengo na kufikiri kiyanikifu na kiubunifu.

3.6 Kutumia stadi za kushawishi na kufikia maafikiano na wenzake katika masuala mbalimbali kama vile urafiki, biashara na uongozi.

3.7 Kujenga uwezo wa kubuni na kushiriki katika shughuli mbalimbali za sanaa, ususi, usafi, upishi, kilimo na ufugaji, ushoni na udobi.

3.8 Kutunga na kuonyesha kazi za muziki na sanaa za maonyesho.

3.9 Kuweza kuchukua tahadhari sahihi wakati wa kutenda stadi mbalimbali katika maisha yake ya kila siku.

## 4.0 MUUNDO WA KARATASI YA UPIMAJI

4.1 Upimaji wa Stadi za Kazi, Haiba na Michezo utakuwa na sehemu A na B. Sehemu A itahusisha Stadi za Kazi na sehemu B itahusisha Haiba na Michezo.

4.2 Karatasi ya upimaji itakuwa na jumla ya maswali **ishirini na tano (25)**.

4.3 Muda wa kufanya upimaji utakuwa saa **1:00** ambapo watahiniwa wasioona watapimwa kwa muda wa saa **1:10**.

## 4.4 SEHEMU A: STADI ZA KAZI

4.4.1 Sehemu hii itakuwa na maswali **kumi na tano (15)**. Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **yote**. Kila swali litakuwa na alama **mbili (02)** na hivyo kufanya jumla ya alama **thelathini (30)** katika sehemu hii.

4.4.2 Maswali katika sehemu hii yatakuwa kama ifuatavyo:

4.4.2.1 **Swali la 1-7** yatakuwa maswali ya kuchagua jibu sahihi kutoka katika chaguzi A, B, C na D.

4.4.2.2 **Swali la 8-12** yatakuwa maswali ya kuoanisha Fungu A na Fungu B.

4.4.2.3 **Swali la 13-15** yatakuwa maswali ya kujaza nafasi zilizoachwa wazi.

## 4.5 SEHEMU B: HAIBA NA MICHEZO

4.6.1 Sehemu hii itakuwa na maswali **kumi (10)**. Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **yote**. Kila swali litakuwa na alama **mbili (02)** na kufanya jumla ya alama **ishirini (20)** katika sehemu hii.

4.6.2 Maswali katika sehemu hii yatakuwa kama ifuatavyo:

4.6.2.1 **Swali la 16-22** yatakuwa maswali ya kuchagua jibu sahihi kutoka katika chaguzi A, B, C na D.

4.6.2.2 **Swali la 23-25** yatakuwa maswali ya kujaza nafasi zilizoachwa wazi.

## 5.0 MADA ZITAKAZOPIMWA

Mada zifuatazo zitapimwa:

### 5.1 STADI ZA KAZI

5.1.1 Usanii wa picha, chapa, maumbo na mapambo
5.1.2 Ususi
5.1.3 Ushoni wa nguo
5.1.4 Sanaa za maonyesho
5.1.5 Muziki
5.1.6 Kilimo, ufugaji na uvuvi
5.1.7 Upishi
5.1.8 Udobi.

### 5.2 HAIBA NA MICHEZO

5.2.1 Uchezaji wa michezo sahili
5.2.2 Jimnastiki
5.2.3 Maadili na utu
5.2.4 Mawasiliano, uhusiano na ushirikiano
5.2.5 Kulinda na kutunza afya
5.2.6 Haki na wajibu.
5.2.7 Matatizo na matendo hatarishi
5.2.8 Fikra makini, uamuzi wa busara na mpango mzuri
5.2.9 Ubunifu, ujasiriamali na rasilimali
5.2.10 Uchezaji wa michezo ya asili
5.2.11 Uchezaji wa michezo ya riadha
5.2.12 Uchezaji wa michezo ya mpira.

## 07 TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA)

### 1.0 UTANGULIZI

Fomati hii ya upimaji wa somo la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) inatokana na Muhtasari wa somo la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa mwaka 2005 ulioanza kutumika 2007. Somo hili litapimwa kwa watahiniwa wenye walimu na vifaa watakaojisajili kufanya somo hili.

### 2.0 MALENGO YA JUMLA

Upimaji wa somo la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) unalenga kubaini uwezo wa mtahiniwa katika:

2.1 Kutambua mbinu mbalimbali za kutafuta na kupata habari kutoka vyanzo mbalimbali.

2.2 Kujenga uwezo wa kutumia teknolojia ya asili na ya kisasa kupata maarifa na ujuzi.

2.3 Kutambua umuhimu wa matumizi ya technolojia ya habari na mawasiliano katika mchakato wa kufundisha na kujifunza.

2.4 Kutambua umuhimu wa technolojia ya habari na mawasiliano katika ukuzaji wa maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

### 3.0 UJUZI WA JUMLA

Mtahiniwa anatarajiwa kujenga ujuzi ufuatao:

3.1 Kuonyesha uwezo wa kutumia Picha, Michoro, Alama na Ishara mbalimbali katika mawasiliano.

3.2 Kuonyesha ujuzi wa kutumia simu.

3.3 Kuonyesha ujuzi wa kutumia njia/mbinu za mawasiliano za asili na kisasa.

3.4 Kuonyesha uelewa wa kutumia Maktaba.

3.5 Kuonyesha uelewa wa kutumia vituo vya habari.

3.6 Kuonyesha uelewa wa kutumia vyombo vya habari.

3.7 Kuonyesha ujuzi wa kutumia Kompyuta kama chombo cha mawasiliano.

## 4.0 MUUNDO WA KARATASI YA UPIMAJI

4.1 Upimaji wa somo la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) utakuwa na sehemu A, B, C na D zenye jumla ya maswali **ishirini na tano (25)** na mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **yote**.

4.1.1 **Sehemu A** itakuwa na maswali **kumi (10)** ya kuchagua chaguzi A, B, C na D. Kila swali litakuwa na alama **mbili (02)** na hivyo kufanya jumla ya alama **ishirini (20)** katika sehemu hii.

4.1.2 **Sehemu B** itakuwa na maswali **matano (05)** ya kuoanisha Fungu A na Fungu B. Kila swali litakuwa na alama **mbili (02**) na kufanya jumla ya alama **kumi (10)** katika sehemu hii.

4.1.3 **Sehemu C** itakuwa na maswali **matano (05)** ya KWELI au SI KWELI. Kila swali litakuwa na alama **moja (01)** na kufanya jumla ya alama **tano (05)** katika sehemu hii.

4.1.4 **Sehemu D** itakuwa na maswali **matano (05)** ya kujaza nafasi zilizoachwa wazi. Kila swali litakuwa na alama **tatu (03)** na kufanya jumla ya alama **kumi na tano (15)** katika sehemu hii.

4.2 Muda wa upimaji utakuwa saa **1:00** ambapo watahiniwa wasioona watapimwa kwa muda wa saa **1:10**.

## 5.0 MADA ZITAZOPIMWA

5.1 Kuchora, kutambua na kutafsiri habari katika picha na michoro
5.2 Kusikiliza
5.3 Simu
5.4 Njia za mawasiliano
5.5 Mawasiliano kwa njia ya maandiko
5.6 Mawasiliano kwa njia ya alama
5.7 Matumizi ya Maktaba
5.8 Matumizi ya vituo vya habari na mawasiliano

5.9 Matumizi ya vyombo vya habari
5.10 Kompyuta na matumizi yake.